CHUO CHA USTAWI WA JAMII

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO



# JARIDA LA MTANDAONI

JANUARI - MACHI, 2025



Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Sotco Komba akitoa hotuba katika Mkutano wa mapitio ya mitaala

## MKUTANO WA MAPITIO YA MITAALA

Tarehe 24, Januari 2025 Katika kampasi ya Dar es Salaam, Chuo cha Ustawi wa Jamii kimewakutanisha wawakilishi wa mashirika ya kitaifa na kimataifa, pamoja na wahadhiri na wanafunzi wa Chuo cha Ustawi Wa Jamii kujadili mapitio ya mitaala.

Akizungumza katika mkutano huo Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Prof. Sotco Komba alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya taasisi za elimu na wadau wa maendeleo ya jamii ili kuhakikisha mitaala hiyo inakidhi mahitaji ya sasa ya kijamii na soko la ajira.

Miongoni mwa masuala muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja na uboreshaji wa mitaala ili iendane na mabadiliko ya kijamii na teknolojia, kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali, na kukuza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika ufundishaji na kufanya tafiti.



Wawakilishi wa Mashirika na wanafunzi waliohudhuria Mkutano wa mapitio ya mitaala



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni (katikati), Mshauri wa Wanafunzi Dr Andrew Randa (Kushoto) na Mwakilishi Kutoka UNESCO Tanzania
Bi Numbilya (kulia) katika picha ya pamoja na Wanafunzi Waelimisha Rika

# WANAFUNZI WAELIMISHA RIKA (PEER EDUCATORS) WAFUZU MAFUNZO ISW

Mkuu wa chuo Dkt. Joyce Nyoni ametunuku vyeti kwa wanafunzi Waelimisha Rika "peer educators" ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii waliopata mafunzo ya kuelimisha rika yaliyoandaliwa na UNESCO Tanzania kwa Kushirikiana na Chuo cha Ustawi wa Jamii chini ya mradi wa O3 Plus.

Dkt. Joyce aliwatunuku vyeti wanafunzi hao katika Hafla ya kuhitimisha Mafunzo ya Waelimisha Rika katika masuala ya Jinsia, Kuzuia ukatili wa kijinsia na UKIMWI, ambayo ilifanyika tarehe 04 Februari, 2025 katika kampasi ya Dar es Salaam.

Wanafunzi 20 walifuzu mafunzo hayo, Kabla ya kutunuku vyeti Dkt. Joyce aliwapongeza wanafunzi hao kwa kutenga muda wao kujifunza masuala ya Kuzuia Ukatili wa kijinsia na UKIMWI. "Ninawasihi mkawasaidia wanafunzi wenzenu, hasa wa ngazi ya Cheti, kwa kuwaelimisha juu ya masuala ya kuzuia Ukatili wa Kijinsia na UKIMWI." alisema Dkt. Joyce Nyoni -Mkuu wa Chuo



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni katika picha ya pamoja na mwanafunzi muelimisha Rika

Mafunzo hayo yamewajengea uwezo na kuwapa maarifa wahitimu ambao watakuwa mstari wa mbele katika kuwaelimisha wanafunzi juu ya masuala ya mahusiano, kuzuia ukatili ya Kijinsia na UKIMWI.



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akiongoza kikao cha Baraza la Wafanyakzi ISW

# WATUMISHI WAJADILI CHANGAMOTO NA UFANISI ISW

Wawakilishi wa watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wameketi kikao cha 19 cha Baraza la Wafanyakazi chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni, 05 Februari, 2025 katika kampasi ya Dar es Salaam.

Kikao hiki kiliwakutanisha wafanyakazi wa chuo pamoja na wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi kwa ajili ya kujadili masuala muhimu ya maendeleo ya taasisi na ustawi wa wafanyakazi.

Miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa ni tathmini ya utekelezaji wa mipango na miradi 2024/2025 Washiriki wa kikao walijadili kwa kina masuala hayo kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na kuhakikisha Taasisi inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.



Wafanyakazi wa ISW wakisikiliza wasilisho la kikao cha Baraza la Wafanyakazi ISW



Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Sotco Komba akiwaongoza Wajumbe kutoka NACTVET katika Ukaguzi wa miundombinu ya ISW

## NACTVET WAFANYA UKAGUZI WA MIUNDOMBINU ISW

NACTVET watembelea Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Dar es Salaam tarehe 19 Februari 2025 na kufanya ukaguzi na tathmini wa miundombinu ya chuo. Zoezi hili lilifanyika ikiwa ni maandalizi ya NACTVET kutoa idhibati ya kuanzishwa kwa programu mpya za masomo katika Chuo cha Ustawi wa Jamii



Picha ya pamoja ya Uongozi wa Chuo na Wajumbe Kutoka NACTVET



Mweneyekiti wa Bodi Bi. Sofia Simba akiwa ameambatana na Wajumbe wa Bodi katika ukaguzi wa miundombinu ya kampasi ya Kisangara

# BODI YA MAGAVANA ISW YAKAGUA MAENDELEO KAMPASI YA KISANGARA

Bodi ya Magavana ya Chuo cha Ustawi wa Jamii Chini ya Uenyekiti wa Bi. Sofia Simba, tarehe 25 Februari, 2025 ilitembelea na Kukagua Miradi ya maendeleo na Miundombinu ya Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kisangara, Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Mwenyekiti wa Bodi Bi. Sofia Simba pamoja na Wajumbe wa Bodi hiyo wameipongeza Menejimenti ya Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa iliyofanyika ya kukamilisha ujenzi wa Mabweni ya wanafunzi, bwalo la kulia chakula, Uboreshaji wa maktaba ya kusomea, kuongeza ofisi za watumishi na Kuongeza Wahadhiri pamoja na Watumishi waendeshaji katika kampasi ya Kisangara kama ilivyowasilishwa katika ripoti ya Meneja wa kampasi.



Picha ya pamoja ya Bodi ya Magavana na Wafanyakazi wa ISW kampasi ya Kisangara



Wafanyakazi wa kampasi ya Kisangara katika hafla ya kufungua mwaka iliyofanyika Kisangara, Mwanga tarehe 26 Februari,2025

## WATUMISHI ISW WAUKARIBISHA MWAKA 2025

Ni ada kwa watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii kupata chakula cha mchana katika hafla ya kuukaribisha mwaka mpya, Mwaka huu 2025 katika Kampasi ya Kisangara tarehe 26 Februari, 2025 na kampasi ya Kijitonyama tarehe 28 Februari, 2025 katika hafla hizo wafanyakazi walipata wasaa wa kushiriki michezo mbalimbali kwa pamoja na kupata chakula cha mchana.

Aidha Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Dr Joyce Nyoni – Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii alitoa vyeti vya pongezi kwa wafanyakazi wa muda mrefu na wafanyakazi bora kutoka katika kila kurugenzi.

Dkt. Joyce Nyoni akitoa neno la kukaribisha mwaka alisema “kasi na ari ya watumishi kuchapa kazi isipungue katika mwaka 2025 tushirikiane kwa pamoja kujenga chuo chetu kuwa bora zaidi”.



Wafanyakazi wa kampasi ya Kijitonyama katika hafla ya kufungua mwaka iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 28 Februari, 2025



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akiongea na Angel Raymond pamoja na wanafunzi wenzake kutoka shule ya Sekondari Kiranyi ya jijini Arusha kuhusu mambo mbali mbali ya kitaaluma, familia na kijamii.

# MAONESHO KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

Chuo cha Ustawi wa Jamii kilishiriki Maonesho Kuelekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake yaliyofanyika jijini Arusha katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid kuanzia tarehe 3 Machi, 2025 na kutamatika tarehe 8 Machi, 2025. Katika maonesho hayo Chuo Cha Ustawi wa Jamii kilielezea na kuonesha umuhimu na umahiri wa ufundishaji wa kozi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ambapo baadhi ya vifaa vinavyotumika kufundishia katika darasa mfano la kozi hii vilioneshwa na kutolewa maelezo katika banda la ISW

Kozi ya malezi, Makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto inayotolewa ISW inaandaa walezi na wasimamizi wa vituo vya kulea watoto ambao wanasimamia usalama wa mtoto, elimu ya awali, saikolojia ya mtoto, ubunifu, mbinu za malezi ya mtoto, afya na lishe na uchangamshi wa awali wa mtoto.



Wanafunzi wa Wanaosoma kozi ya maendeleo ya Jamii za kikanda kutoka Chuo kikuu cha Oslo metropolitan university (Norway) wakifurahia kuona jinsi Banda la ISW lilivyo sheheni vifaa vya kujifunzia kozi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya mtoto.

''Tumevutiwa sana na Kozi hii sisi tunashule za awali na msingi kwahivyo elimu hii ya makuzi na malezi ni muhimu sana tunaiihitaji" alisema katibu wa wamiliki wa shule binafsi Arusha



Watumishi Wanawake wa ISW kutoka kampasi ya Kisangara, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yaliyofanyika Arusha

# WANAWAKE WA ISW WASHEREHEKEA SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE 2025

Watumishi wanawake wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara na Dar es Salaam washerehekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake, ambapo Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika Arusha katika Uwanja Sheikh Amri Abeid na kuhudhuriwa na watumishi kutoka Kampasi ya Kisangara mgeni rasmi akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa Dar es Salaam maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Leaders Club na kuhudhuriwa na Watumishi kutoka kampasi ya Dar es Salaam, huku mgeni rasmi akiwa ni Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Maadhimisho hayo yalibeba kauli mbiu isemayo "Wanawake na Wasichana 2025, Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji"




Watumishi Wanawake wa ISW kutoka kampasi ya Kijitonyama, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yaliyofanyika Dar es Salaam



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ikikagua Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara ISW

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YATEMBELEA NA KURIDHISHWA NA MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MIHADHARA ISW

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Fatma Toufiq, ilitembelea mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wa Chuo cha Ustawi wa Jamii kampasi ya Dar es Salaam tarehe 17 Machi, 2025.

Baada ya ukaguzi kamati iliridhishwa na ubora wa mradi huo, muda na gharama iliyotumika ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 38 ukijengwa kwa fedha za mapato ya ndani. "Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2025, ambapo ukumbi huo utaweza kuhudumia wanafunzi 419 kwa wakati mmoja" alisema Dkt Joyce Nyoni - Mkuu wa Chuo ISW.



Muonekano wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara ISW

“Nimeridhishwa na maendeleo ya mradi huu na niwapongeze Mkuu wa Chuo Dkt Joyce Nyoni na Menejimenti ya Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ya Kusimamia mradi huo kwa Fedha za ndani” alisema Mhe Fatma Toufiq - Mwenyekiti wa Kamati.

Kamati imeahidi kuwasilisha bungeni pendekezo kwa serikali kuongeza fedha katika mradi huo ili fedha hizo zikasaidie katika ukamilishaji wa Ujenzi kwa haraka na katika ubora.

# KURASA RASMI ZA CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**INSTAGRAM**
**@ISW_OFFICIAL_TZ**

**TWITTER (X)**
**@TAASISIYAUSTAWI**

**WHATSAPP CHANNEL**
**@CHUO CHA USTAWI WA JAMII**

**YOUTUBE CHANNEL**
**@ISW_OFFICIAL_73**

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

Institute of Social Work
210 Shekilango Road
P.O. BOX 3375
14113 Kijitonyama
Dar es Salaam
+255735509090
+255677111200
+255716121096
rector@isw.ac.tz
or
info@isw.ac.tz